Jarida La

# MIFUGO NA UVUVI

#mifugonauvuviniutajiri

TOLEO NO; WMU 017| 2025 WWW.MIFUGOUVUVI.GO.TZ | KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
MINISTRY OF LIVESTOCK AND FISHERIES

## Meli ya kwanza ya Uvuvi wa Bahari Kuu yazinduliwa




Aprili 2026

Scan hapa Kusoma taarifa za Tovuti yetu

@Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Jarida la Mtandaoni

HALIUZWI



# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

@Wizara ya Mifugo na Uvuvi

# Yaliyomo


1 Bodi ya Uhariri............**Uk. 04**

2 Historia yaandikwa! Rais Samia azindua meli ya uvuvi Bahari Kuu ............**Uk. 05**

3 Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) kufanyiwa tathmini Upya.......**Uk 06**

4 Wakaguzi watakiwa kusafirisha kwa wingi mazao ya uvuvi nje ya nchi... **Uk. 07**

5 Shilingi Bil.30.8 kutumika kwenye chanjo na utambuzi wa mifugo 2026/2027.......... **Uk. 08**

6 Vijana 200 kunufaika na fursa za unenepeshaji wa mbuzi na kondoo........... **Uk. 9-10**

7 Matukio katika picha... **UK. 11**

8 Shilingi Bil 30.7 kuwanufaisha vijana BBT ....... **Uk. 12**

9 Serikali kuimarisha tasnia ya kuku...... **Uk. 13**

10 Elimu ya nadharia na vitendo yatolewa kwa wafugaji..... **Uk. 14**

11 Mabalozi wateule wahimizwa kuzinadi fursa za mifugo na uvuvi kimataifa...... **Uk. 15**

12 Serikali yapokea mtambo wa kisasa kuimarisha sekta ya uvuvi............**Uk. 16**

13 Bi. Meena ahimiza ushirikiano kuinua sekta ya mifugo .......**Uk. 17**

14 Matukio katika picha........ **Uk. 18**

15 Mtaala wa wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa wajadiliwa ...**Uk. 19**

16 Chanjo Milioni 2 zakabidhiwa kutokomeza Sotoka ya mbuzi na kondoo ...**Uk. 20**












# Bodi ya Wahariri:


### Mwenyekiti
**Mbaraka Kambona**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

### Wahariri
**Elibariki Mafole -** Afisa Habari Mwandamizi
**Hamis Hussein**- Afisa Habari

### Msanifu
**Fausta Njelekela**- Afisa Habari

### Wajumbe
**Omary Mtamike -** Afisa Habari Mwandamizi
**Stanlay Brayton -** Afisa Habari
**Chiku Makwai-** Afisa Habari
**Martha Mbena** - Mkutubi

# Historia yaandikwa! Rais Samia azindua Meli ya Uvuvi Bahari Kuu

**Na, Omary Mtamike**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amezindua meli ya kwanza ya uvuvi wa bahari kuu ambayo itaiwezesha nchi kuvua samaki waliopo kwenye ukanda wa maalum wa uchumi wa bahari (EEZ) ambao awali haukuweza kufikiwa kutokana na kukosekana kwa meli ya aina hiyo.

Hafla hiyo ya uzinduzi imefanyika Aprili 25,2026 kwenye ufukwe wa makao makuu ya Shirika la Uvuvi nchini (TAFICO) Kigamboni mkoani Dar-es-salaam ambapo Mhe. Rais Samia amesema kuwa hatua hiyo inalenga kukuza fursa za ajira, kuongeza mapato ya serikali na kuboresha lishe. "Niipongeze serikali ya Japan kwa kushirikiana nasi katika kutengeneza meli hii na kupitia wao kwa kushirikiana na UNDP tutapata boti mbili za kasi ambazo zitasimamia doria ya uvuvi wa bahari kuu." Ameongeza Mhe. Rais Samia.

Aidha, Rais Samia amesisitiza kuwa serikali itaendelea kuboresha sekta ya uvuvi kupitia ujenzi wa bandari za uvuvi ikiwemo ya kilwa ambayo imefikia asilimia 97 na Bagamayo ambazo zote kwa pamoja zinalenga kuimarisha uchumi, ajira na usalama wa chakula.

"Sambamba na hilo tutaimarisha mafunzo na tafiti za kitaalam ili kuhakikisha rasilimali za bahari zinasimamiwa kwa ufanisi na misingi endelevu kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo." Amesema Mhe. Rais Samia

Aidha Mhe. Rais Samia ametoa maelekezo mbalimbali kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikiwa ni pamoja na kutunza meli hiyo, kutatua changamoto za wavuvi wadogo zinazohusu mitaji na mazingira ya kufanya shughuli zao, kutoa elimu ya usimamizi wa fedha kwa wavuvi ili fedha wanazopata ziwanufaishe na kutumia sheria na taratibu kwenye usimamizi wa uvuvi endelevu na badala ya nguvu na mabavu.

Akizungumza awali, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa amemshukuru Rais Samia kwa jitihada za kuendeleza sekta ya uvuvi nchini ambapo ameeleza kuwa meli hiyo ni sehemu ya meli nyingine 4 zinazotarajiwa kununuliwa na serikali ili ziimarishe uvuvi wa bahari kuu.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizindua Meli ya kwanza ya Uvuvi wa Bahari Kuu TAFICO FV.01 Aprili 25,

# PROGRAMU YA KUENDELEZA KILIMO NA UVUVI (AFDP) KUFANYIWA TATHMINI UPYA

**Na, Hamisi Hussein**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa Aprili 2, 2026 amepokea taarifa ya utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) kwa kipindi cha Julai 2022- Machi 2026 inayotekelezwa na serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo ( IFAD), kikao kilichofanyika ofisi ndogo za wizara zilizopo Kambarage Tower, jijini Dodoma.

Programu hiyo inayojikita kuongeza tija na faida katika mbegu za kilimo, uvuvi na ukuzaji viumbe maji, kuboresha upatikanaji wa masoko, kuongeza thamani ya mazao pamoja na kuendeleza sekta binafsi, inagharimu kiasi cha dola za marekani milioni 77.416 ulianza kutekelezwa Julai 2021 na utakamilika Desemba 2027.

Pamoja na mambo mengine, baada ya kupokea taarifa hiyo, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru ameielekeza timu ya wataalam inayotekeleza programu hiyo kutoka wizarani kutathmini kwa kina sababu zilizochelewesha mradi huo hususani mchakato wa zabuni.

Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) inatarajiwa kunufaisha kaya 260,000 ambapo takribani watu milioni 1.3 wakiwemo wakulima, wazalishaji wadogo na wakati wa mbegu na pembenjeo za kilimo, wavuvi wadogo, wachakataji wa mazao ya uvuvi, wakuzaji viumbe maji na wachakataji wa mwani kutoka halmashauri 46 za mikoa 12 ya Tanzania Bara na Zanzibar watanufaika.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa akizungumza na Timu ya Wataalam inayoratibu Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) kutoka wizarani wakati akipokea taarifa ya utekelezaji wa programu hiyo, kikao kilichofanyika Aprili 2, 2026 Kambarage Tower, Dodoma.




Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Prof. Mohammed Sheikh (katikati waliokaa) akiwa kwenye picha ya pamoja na washiriki wa mafunzo ya ubora kwa maafisa wakaguzi wa mazao ya uvuvi yaliyofanyika katika Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani tarehe 8 Aprili, 2026.

# WAKAGUZI WATAKIWA KUSAFIRISHA KWA WINGI MAZAO YA UVUVI NJE YA NCHI

**Na, Maria Mtambalike**

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Prof. Mohammed Sheikh amewataka wakaguzi wa mazao ya uvuvi kufanya kazi zao kwa ubora ili kulisaidia taifa kuongeza kiwango cha mazao ya uvuvi yanayosafirishwa nje ya nchi.

Prof. Sheikh ametoa kauli hiyo Aprili 8, 2026 wakati akizindua mafunzo ya siku tano kwa maafisa wakaguzi wa mazao ya uvuvi 25 yaliyoandaliwa na Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO). Mafunzo hayo yallifanyika katika Wilaya Bagamoyo, mkoani Pwani.

"Takwimu zinaonesha kwasasa tunasafirisha tani 60,000 pekee za samaki kwenda nje ya nchi hivyo uwepo wa mafunzo haya uwe chachu ya kuongeza ubora utakaosaidia taifa kuongeza kiasi cha samaki kinachopelekwa nje ya nchi." Amesema Prof. Sheikh

Akiongea Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), Dkt Semvua Mzighani amesema mafunzo haya yamelenga kuwajengea uwezo maafisa ukaguzi wa mazao ya uvuvi juu ya taratibu za ukaguzi wa mazao ya uvuvi pamoja na viwango vya ubora vya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Pia amewasihi washiriki wa mafunzo kuzingatia mafunzo watakayopatiwa na elimu watakayoipata kupitia mafunzo hayo ikawasaidie wananchi katika maeneo yao.

Awali mratibu wa mafunzo hayo, Mkufunzi Anold Mbunda amesema hii ni awamu ya kwanza ya mafunzo ambapo imejumuisha washiriki kutoka ukanda wa pwani, awamu ya pili ya mafunzo haya itafanyika mkoani Kigoma ambapo itahusisha washiriki kutoka kanda ya ziwa.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, **Mhe. Ng'wasi Kamani** akijibu Maswali Bungeni Aprili 09, 2026.

# SHILINGI BIL. 30.8 KUTUMIKA KWENYE CHANJO NA UTAMBUZI WA MIFUGO 2026/2027

**Na, Hamisi Hussein**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imetenga shilingi bilioni 30.8 ili kuendelea na awamu ya pili ya Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Hayo yameelezwa Aprili 09, 2026 Bungeni Jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Ng'wasi Kamani wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Arusha, Mhe. Marirta Gido Kivunge lililohoji, je serikali ina mpango gani wa kutoa huduma za dawa na chanjo muhimu ilikuboresha afya na kuwaongezea thamani mifugo?

Mhe. Kamani amesema serikali inaendelea na mpango wa kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kutekeleza Mpango wa Chanjo na Utambuzi wa Mifugo wa miaka mitano wenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 216, unaotekelezwa kuanzia 2024/2025 hadi 2028/2029.

"Mheshimiwa Mwenyekiti katika bajeti ya Mwaka 2024/2025, serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 61.2 kwa ajili kuendesha kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 uchanjaji umefikia asilimia 64.5 kwa nchi nzima" alisema Mhe. Kamani.

Ameongeza kuwa katika awamu ya pili ya kampeni hiyo ya chanjo, wizara imefanya tathmini ya magonjwa 13 ya kipaumbele ambayo yatazingatiwa ikiwemo Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD) ambapo hadi sasa kuna aina nne vya virusi ambavyo vimeshafanyiwa tathmini itakayosaidia kutambua aina

> **Mheshimiwa Mwenyekiti katika bajeti ya Mwaka 2024/2025, serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 61.2 kwa ajili kuendesha kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 uchanjaji umefikia asilimia 64.5 kwa nchi nzima.**
>
> **Mhe. Ng'wasi Kamani**
> **Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi**





Naibu Katibu Mkuu (Mifugo) Dkt. Fabian Madele akizungumza na wadau wa sekta ya mifugo, kuhusu mradi wa Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) ya unenepeshaji wa mbuzi na kondoo Wilayani Kongwa, Aprili 9, 2026

# VIJANA 200 KUNUFAIKA NA FURSA ZA UNENEPESHAJI WA MBUZI NA KONDOO

**Na, Stanley Brayton**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inayotekeleza mradi wa miaka mitano wa Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) ya unenepeshaji wa mbuzi na kondoo katika eneo la kituo cha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) iliyopo wilayani Kongwa, imepanga kuwawezesha vijana 200 wa kitanzania kupata mafunzo hayo ikiwa na lengo la kuongeza ushiriki wa vijana na wanawake katika ujasiliamali wa biashara ya mifugo.

Akizungumza Aprili 9, 2026 wilayani Kongwa Jijini Dodoma kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Naibu Katibu Mkuu (Mifugo), Dkt. Fabian Madele, wakati wa warsha ya utambulisho wa mradi huo, amesema mradi huo una thamani ya takribani shilingi billioni 81 na unalenga kuwawezesha vijana kupitia shughuli za unenepeshaji wa mbuzi na kondoo kibiashara, uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho, uchakataji wa vyakula vya mifugo, pamoja na matumizi ya teknolojia za kisasa.

"Walengwa wakuu wa mradi huu ni vijana, ambao kupitia utekelezaji wake watapata ujuzi na uzoefu wa vitendo katika mnyororo mzima wa thamani wa mazao ya mifugo, hususan mbuzi, na kupitia mafunzo haya, vijana wetu watajengewa uwezo wa kuingia kwenye biashara za kisasa za mifugo na hivyo kujiongezea kipato pamoja na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa." amesema Dkt. Madele

Aidha, Dkt. Madele amesema baada ya vijana kupata ujuzi huo, matarajio ya serikali ni kuwa vijana wataweza kujiajiri wenyewe, kuanzisha biashara zao, na kuwa sehemu ya suluhisho la changamoto ya ajira nchini, ambapo vijana watakaonufaika watakuwa na fursa ya kupatiwa mikopo isiyo na dhamana kwa ajili ya kuendeleza biashara zao baada ya mafunzo.

Vilevile, Dkt. Madele amebainisha kuwa matokeo ya kuwepo kwa mradi huo ni kutokana na uongozi madhubuti wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutambua kwa kina changamoto ya ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana, ndiyo maana Mheshimiwa Rais amechukua juhudi za makusudi kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kwa ajili ya kuboresha maisha ya vijana kupitia miradi yenye tija kama huo wa BBT.

>> > KUTOKA UK. 09

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Ufuatiliaji na Tathmini kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ndg. Daudi Mayeji amesema mradi huo hautaishia kwa vijana waliopo Dodoma tu bali kwa vijana kutoka maeneo mbalimbali ya nchi, ambapo mpango huo utamuwezesha kijana kuhudumia mbuzi 100 kwa pamoja.

Pia, Ndg. Mayeji amesema mradi huo unategemea ndani ya miaka mitano kutoa mafunzo kwa vijana takriban 1750 na serikali tayari imeshatenga eneo la hekta 2000 kwa ajili ya kupanda malisho ya mifugo.

Naye, Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, ambaye ni Afisa Tarafa ya Kongwa, Ndg. Jeremiah Kabebwa ameishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuwaletea mradi wenye fursa kwa vijana ambapo ameihakikishia wizara kuwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya itahakikisha vijana wote wanaichangamkia fursa hiyo ili kuweza kujikwamua kiuchumi.

*Walengwa wakuu wa mradi huu ni vijana, ambao kupitia utekelezaji wake watapata ujuzi na uzoefu wa vitendo katika mnyororo mzima wa thamani wa mazao ya mifugo, hususan mbuzi, na kupitia mafunzo haya, vijana wetu watajengewa uwezo wa kuingia kwenye biashara za kisasa za mifugo na hivyo kujiongezea kipato pamoja na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa.*

**Dkt. Fabian Madele**
Naibu Katibu Mkuu Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Mifugo)





# MATUKIO KATIKA PICHA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na Viongozi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wakati wa uzinduzi wa meli ya Uvuvi Aprili 2026.







# SHILINGI BIL. 30.7 KUWANUFAISHA VIJANA PROGRAMU YA BBT

**Na, Hamis Hussein**



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Ng'wasi Kamani akijibu maswali ya Wabunge , Bungeni Aprili 10, 2026.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Ng'wasi Kamani amesema serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Jenga Kesho Iliyobora (Building Better Tomorrow - BBT) ambapo katika mwaka wa fedha 2025/2026 wizara hiyo imepokea shilingi bilioni 30.7 (sekta ya uvuvi shilingi bilioni 25.9 na sekta ya mifugo shilingi bilioni 4.75) kwa ajili ya kuwawezesha vijana katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mhe.Kamani amesema hayo Aprili 10, 2026 Bungeni Jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Vitimaalum, Mhe. Maryam Azan Mwinyi, kwenye Kipindi cha Maswali na Majibu cha Bunge la 13, Mkutano wa Tatu, Kikao cha Sita.

Swali la Mbunge huyo lilihoji hatua inayochukuliwa na serikali kuwawezesha wananchi hususani vijana na wavuvi wadogo kushiriki kikamilifu katika uchumi wa Bluu.

"Mheshimiwa Spika, Kupitia programu ya BBT, vijana 308 wamepatiwa mikopo isiyo na riba na yenye masharti nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ufugaji wa samaki kwenye vizimba, ufugaji wa majongoo bahari, unenepeshaji kaa na kilimo cha mwani" alisema Mhe. Kamani

Aidha, ameongeza kuwa, serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) inaendelea kutekeleza zoezi la utoaji wa mikopo isiyo na riba na yenye masharti nafuu kwa wavuvi wadogo wakiwemo vijana kwa kuwawezesha kupata nyenzo za uvuvi zikiwemo maboti ya kisasa pamoja na nyavu za uvuvi.



Vizimba vya Samaki Kisoko, Mwanza



# SERIKALI KUIMARISHA TASNIA YA KUKU

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa

**Na, Stanley Brayton**

Serikali kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya kuku imepanga kuleta mabadiliko yenye tija ili kuongeza uzalishaji nchini ambao utasaidia kuinua vipato vya wananchi na taifa kiujumla.

Akizungumza Aprili 11, 2026 Jijini Dodoma katika kikao cha mkakati wa kuimarisha tasnia ya kuku ambacho kiliwahusisha viongozi na wadau wa mnyororo wa thamani hiyo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa amesema uzalishaji kuku unatakiwa kupewa kipaumbele kwani ndio inagusa maisha ya kila mwananchi na chakula chenye usalama kinapopatikana, hivyo ni vyema kufanya mabadiliko ili wafugaji wafuge kisasa kuendana na teknolojia iliyopo sasa.

***"Ili kunyanyua uchumi wetu ni lazima kutanua wigo wa tasnia ya kuku kwa kutumia teknolojia mbalimbali, maana tunaweza zalisha kwa wingi mazao ya kuku na kwa ubora zaidi na kuuza nchi za nje na kupata fedha za kigeni pamoja na kukuza mashirikiano ya kidiplomasia baina ya nchi yetu na nchi zingine." Amesema Mhe. Balozi Dkt. Bashiru***

Aidha, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru amesema ana uhakika kuwa tasnia ya kuku inaweza kuimarika zaidi ili kuwahudumia wananchi wengi, na ndio maana wizara ipo katika Mapitio ya Sera za Mifugo na Uvuvi ili kuziboresha na kuhakikisha zinaendana na Dira ya Taifa ya 2050.

Pia, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru amewataka Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) kujenga maabara ya kupima vyakula vya mifugo ili kuwezesha usalama wa chakula cha Mifugo. Wataalam, wizara na taasisi za serikali kuendelea kukutana na wadau mbalimbali wa tasnia ya kuku na kusaidiana nao katika kukuza sekta hiyo ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Kisaka Meena amesema kuwa tasnia ya kuku ni muhimu na ndio maana serikali inasimama kwa ukamilifu katika kuhakikisha inakuwa kwa kasi na kuwanufaisha wananchi. Vilevile amesema kikao hicho kitasaidia katika kutatua changamoto za kuku na wafugaji ili waweze kufuga kwa urahisi na kupata chakula cha kuku kiurahisi na kwa bei nafuu.

# ELIMU YA NADHARIA NA VITENDO YATOLEWA KWA WAFUGAJI

**Na, Stanley Brayton**

Taasisi ya Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA) na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) zimeendelea kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa ili kukuza tasnia ya maziwa kwa kuongeza uzalishaji wa maziwa nchini.



Mkurugenzi Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani (DRTE), Ndg. Samwel Mdachi akihutubia wafugaji wa ng'ombe bozra wa maziwa, Aprili 13, 2026 Tanga.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi Aprili 13, 2026 Jijini Tanga katika ufunguzi wa semina ya wafugaji wa ng'ombe bora wa maziwa kupitia mradi wa Maziwa Faida, Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi (DRTE), Ndg. Samwel Mdachi amesema lengo la mafunzo hayo ni kuongeza uzalishaji wa maziwa nchini na mpango ni kuwafikia wafugaji 3,000 ndani ya miaka mitano (5) ya utekelezaji wa mradi huo, ambapo hadi sasa wafugaji 1,888 wamefikiwa.

"Uboreshaji wa uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa mlionao utasaidia kuongeza kiwango cha uzalishaji wa maziwa bora na hivyo kuongeza kipato katika kaya zenu na ongezeko la maziwa pia litasaidia kuongeza upatikanaji wa mali ghafi kwa ajili ya kuviwezesha viwanda vya kusindika maziwa, hasa kiwanda cha maziwa cha Tanga Fresh ambacho kwa mujibu wa taarifa zilizopo bado kinapata maziwa kidogo ya kusindika kutoka kwa wafugaji walioko mkoani Tanga na mikoa mingine jirani." Amesema Ndg. Mdachi

Aidha, Ndg. Mdachi amebainisha kuwa ili ufugaji hapa nchini uwe na tija na endelevu, ni vizuri kushirikisha kwa karibu kundi kubwa la vijana na wanawake ambao ndiyo wengi na nguzo kuu ya uchumi katika kuimarisha mifumo endelevu ya usalama wa chakula na lishe hapa nchini, barani Afrika na dunia nzima.

Vilevile, Ndg. Mdachi amewapongeza taasisi za LITA na TALIRI kwa namna wanavyoendelea kushirikiana katika kutoa huduma za mafunzo na ushauri elekezi kwa wafugaji na wadau wengine katika sekta ya mifugo hapa nchini na kuwataka kuendeleza ushirikiano huo katika kutoa elimu hiyo katika vituo vingine vilivyoko katika mikoa mingine hapa nchini.

Ndg. Mdachi amewataka wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kutumia vizuri fursa hiyo adimu na adhimu ya kuwezeshwa kupata mafunzo kama hayo kwa msaada mkubwa kutoka nchi ya Ireland kupitia Taasisi za Utafiti na Mafunzo TEAGASC pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, ambayo yanatolewa bila gharama yoyote ambapo wakati mwingine wangelazimika kulipia na wawe tayari kubadilika na kuboresha ufugaji wao na kuwa wenye tija na endelevu.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA), Dkt. Pius Lazaro Mwambene amesema kuwa mafunzo hayo ni mwendelezo wa utekelezaji wa mpango wa utoaji wa mafunzo kwa wafugaji 3,000 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Muheza katika kipindi cha miaka mitano ijayo, tangu kuanza kwa utekelezaji wa mafunzo hayo mwishoni mwa mwaka 2022, ambapo LITA imewafikia washiriki 1,888 (wafugaji ni 1,858 na maafisa ugani 30) na katika awamu hii ya saba ya mafunzo haya yatawafikia wafugaji 310 wakiwemo washiriki 78 na mafunzo hayo yamekuwa yakianza kwa kupokea changamoto zinazowakabili wafugaji ambapo ufumbuzi wa changamoto zao hujadiliwa kwa pamoja na kufundishwa kwa njia rahisi ya nadharia na vitendo.

# MABALOZI WATEULE WAHIMIZWA KUZINADI FURSA ZA MIFUGO NA UVUVI KIMATAIFA

**Na, Hamis Hussein**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa amekutana na Mabalozi Wateule wa Tanzania kwa lengo la kuwafahamisha fursa zilizopo katika sekta za mifugo na uvuvi ili kwenda kuzinadi kwenye Nchi walizopangiwa kuiwakilisha Tanzania ikiwa ni sehemu ya kuimarisha diplomasia ya uchumi kimataifa.

Mhe. Dkt. Bashiru amekutana na mabalozi hao katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Waziri Mkuu Jijini Dodoma leo Aprili 13, 2026 na kuwaeleza kuwa sekta za mifugo na uvuvi zinahitaji kupanua wigo wa masoko ya kimataifa yatakayochochea uzalishaji na ukuaji wa uchumi wa wananchi.

"Kama ambavyo mtakavyokuwa makini na sekta zingine za kiuchumi kama maliasili na utalii, pia sekta za mifugo na uvuvi ni eneo muhimu, nchi yetu bado tuna nafasi ya kujikomboa kiuchumi kutokana na Kilimo, Mifugo na Uvuvi, kwa hiyo uwakilishi wenu unakuwa na mchango mkubwa katika diplomasia ya Uchumi," alisema Mhe. Dkt. Bashiru.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mabalozi Wateule wa Tanzania baada ya kufanya mazungumzo nao Mjini Dodoma Aprili 13, 2026.

Aidha, Mhe. Dkt. Bashiru ameongeza kuwa wizara bado inahitaji mashirikiano na mataifa mengine katika maeneo ya teknolojia na miundombinu ya uzalishaji, mitaji, uwekezaji katika uzalishaji wa vyakula vya mifugo na samaki, afya ya mifugo, kuimarisha mbari (mbegu bora) za mifugo, masoko ya mazao ya mifugo na uvuvi pamoja na mafunzo na utaalam katika sekta hizo, mambo ambayo yatavutia uwekezaji.

Kwa upande wake, Balozi wa Tanzania Nchini Saudi Arabia, Mhe. Eng. Zena Ahmed Saidi akizungumza katika kikao hicho ameiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi kushirikiana kwa karibu na balozi hizo ikiwa ni pamoja na kuwapatia vielelezo vyote ili kupata nguvu ya kuzitangaza sekta hizo kwa wawekezaji wa kimataifa.





# SERIKALI YAPOKEA MTAMBO WA KISASA KUIMARISHA SEKTA YA UVUVI

**Na, Chiku Makwai**

Serikali imepokea mtambo wa kisasa wa kuzalisha barafu na kukaushia dagaa, pamoja na majokofu yanayotumia nishati ya jua, kutoka mradi wa FISH4ACP ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuimarisha sekta ya uvuvi mkoani Kigoma.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano ya mtambo huo iliyofanyika Aprili 14, 2026 katika mwalo wa Katonga mkoani Kigoma, Katibu Tawala wa Mkoa huo, Mhe. Hassan Rungwa, ambaye alikuwa mgeni rasmi, amesema kuwa mtambo huo utawasaidia wavuvi kuongeza ufanisi katika shughuli zao na kukuza uzalishaji utakao wawezesha kukidhi mahitaji ya masoko ya ndani na nje ya nchi.

"Hatua hii itaongeza ubora wa mazao ya uvuvi, kuimarisha ushindani wa bidhaa zetu katika masoko ya ndani na nje ya nchi, pamoja na kuinua kipato cha wananchi wa Mkoa wa Kigoma," amesema Mhe. Rungwa.

Aidha, Mhe. Rungwa amewataka wavuvi pamoja na mamlaka zinazosimamia mradi huo kuhakikisha wanatunza mtambo huo na vifaa vyake ili uweze kudumu na kuwanufaisha wananchi pamoja na serikali kwa ujumla.

Pia Mhe. Rungwa amefafanua kuwa vifaa vilivyokabidhiwa ni pamoja na mtambo wenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya tani 15 za barafu kwa siku na kukaushia zaidi ya kilo 300 za dagaa kwa siku, majokofu 10 yenye uwezo wa kuhifadhi zaidi ya lita 500 kila moja na zaidi ya coolbox 20 zenye uwezo wa kuhifadhi zaidi ya lita 15 kila moja.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Mhe. Prof. Mohammed Sheikh amesema uwekezaji huo utachochea ongezeko la thamani ya mazao ya uvuvi na kuongeza tija katika sekta hiyo.

Aidha, Prof. Sheikh pia amelishukuru Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) kupitia mradi wa FISH4ACP kwa kufanikisha upatikanaji wa mtambo huo, na kuwataka wadau wengine kuendelea kuwekeza katika sekta ya uvuvi ili kukuza uzalishaji.

"Ni muhimu kuongeza uwekezaji katika uzalishaji ili kupunguza uhaba wa mazao ya uvuvi na kukidhi mahitaji ya soko," amesema Prof. Sheikh.

Ameongeza kuwa serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya sekta hiyo ikiwemo ujenzi wa bandari za uvuvi katika maeneo ya Bagamoyo na Kilwa, ambazo zitasaidia kurahisisha mnyororo mzima wa thamani wa mazao ya uvuvi.

Naye Mwakilishi Mkazi wa FAO, Dkt. Nyabenyi Tipo amesema mradi huo ni wa kipekee barani Afrika, ukiwa na uwezo wa kutumia umeme wa gridi ya taifa pamoja na nishati ya jua, hali inayotarajiwa kupunguza gharama za uzalishaji wa barafu kwa hadi asilimia 50.





Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma Mhe. Hassan Rungwa ( wa kwanza kushoto), akikata utepe wakati wa makabidhiano ya mtambo wa kisasa wa kuzalisha barafu na kukausha dagaa, zoezi hilo limeshuhudiwa na Naibu Katibu Mkuu ( Uvuvi) Prof. Mohammed Sheikh, na Mwakilishi wa FAO Nchini Tanzania, Aprili 14, 2026 Kigoma.



Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Watendaji wa sekta ya mifugo wakiwa katika kikao cha kujadili mashirikiano baina yao kilichofanyika Makao Makuu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mtumba jijini Dodoma Aprili 15, 2026

Bi. Agnes Meena
Katibu Mkuu - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

# BI. MEENA AHIMIZA USHIRIKIANO KUINUA SEKTA YA MIFUGO

**Na, Fausta Njelekela**

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agness Meena amekutana na watendaji wakuu wa taasisi na wataalam wa sekta ya mifugo kwa lengo la kujadili kwa pamoja jinsi ya kuongeza ushirikiano ili kubaini na kutatua changamoto zinazowakabili wataalam hao katika utendaji kazi.

Akizungumza wakati wa kikao hicho cha majadiliano na wataalamu wa sekta hiyo, yaliofanyika Aprili 15, 2026 Katika Ukumbi wa Ofisi ya Wizara Jijini Dodoma, Bi. Meena amesema ushirikiano katika sekta ya mifugo utaleta mbinu bora za kutatua changamoto kwa kutumia wataalamu walioko kwenye maeneo ya wafugaji.

"Ushirikiano baina ya viongozi na wataalamu wa sekta ya mifugo utasaidia kutambua changamoto zilizopo na kuzitatua, ili kuongeza thamani ya mazao ya mifugo." Amesema Bi. Meena

Aidha, Bi. Meena, ameweka msisitizo kwa watendaji hao kujikita katika kuongeza ushirikiano ili kutafuta mbinu bora za kuvumbua changamoto na njia bora za kutatua changamoto hizo zinazoikumba sekta ya mifugo kwa kutumia wataalam walioko kwenye maeneo ya wafugaji.

Kwa Upande wake, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Dkt. Fabiani Madele amesema ushirikiano huo ni muhimu ikiwa viongozi na wadau wa kitaaluma wataungana pamoja ili kuendeleza sekta hii ili kuimarisha na kuikuza.

Naye, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo nchini, Dkt. Benezeth Lutege amesema kuwa wizara inatakiwa kuwa na jukumu la kusimamia dawa, chanjo na vifaa tiba na kufuatilia changamoto zinazoikumba sekta ya mifugo ili kuweza kuzitatua kwa haraka zaidi.

Mwenyekiti wa Chama cha Madaktari wa Wanyama Tanzania,(TVA), Prof. Esron Karimuribo, amebainisha changamoto mbalimbali zinazoikumba sekta ya mifugo ikiwemo tatizo la ajira kwa vijana, changamoto ya kuhudhuria mafunzo ya wanagenzi na ameishukuru wizara kwa kuwakutanisha wataalam hao pamoja ili

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA















Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu Dkt. Charles Mhina (mwenye tai ya bluu) akiwa pamoja na wataalamu wa sekta ya mifugo baada ya kikao cha kutoa mapendekezo na kupitisha mtaala wa shamba darasa kwa wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa, kikao kilichofanyika Aprili 28, 2026 Dodoma.

# MTAALA WA WAFUGAJI WADOGO WA NG'OMBE WA MAZIWA WAJADILIWA

**Na, Fausta Njelekela**

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Charles Mhina ambaye ni Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu, ameongoza kikao muhimu kilichowakutanisha wataalamu wa Sekta ya mifugo kutoa mapendekezo na kupitisha mtaala wa shamba darasa utakaowasaidia wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa ili kuboresha shughuli zao za uzalishaji.

Akizungumza katika kikao hicho Dkt. Mhina Aprili 28, 2026 Dodoma amesema mtaala huo unalenga kuimarisha tasnia ya maziwa kwa kuzingatia mnyororo wote wa thamani, kuanzia ngazi ya mzalishaji hadi masoko ya bidhaa za maziwa.

"Mtaala huu lazima uzingatie mahitaji halisi na uhalisia wa hali ya ufugaji nchini ili uweze kutoa maarifa na ujuzi unaoendana na mazingira ya wafugaji wadogo." Amesema Dkt. Mhina

Aidha, Dkt. Mhina amebainisha kuwa ni muhimu kwa wataalamu wa sekta ya mifugo kujihusisha moja kwa moja na shughuli za ufugaji ili kuelewa kwa kina changamoto zinazowakabili wafugaji.

Kwa upande wake Dkt. Zabron Nziku ambaye ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) Kanda ya Mashariki ambaye amezungumza kwa niaba ya washiriki amesema ni lazima mtaala ulenge kutatua changamoto zinazowakumba wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa na kuongeza tija ya ufugaji, hatua itakayochangia kukuza uzalishaji na kuinua kipato cha wafugaji.

Aidha, Dkt. Nziku amemshukuru mgeni rasmi kwa ujumbe wake ulioamsha ari ya washiriki, pia amemhakikishia kuwa maelekezo yote aliyoyatoa yatazingatiwa kikamilifu wakati wa kuchakata na kuuthibitisha mtaala huo.



Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agness Kisaka Meena (katikati), akikabidhiwa dozi ya chanjo ya ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo kutoka kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Hester Bioscience Africa Ltd, Bi. Christine Sokoine

# CHANJO MILIONI 2 ZAKABIDHIWA KUTOKOMEZA SOTOKA YA MBUZI NA KONDOO

**Na, Stanley Brayton**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepokea chanjo dozi milioni mbili kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), kwa ajili ya kutokomeza ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo, ikiwa ni moja ya utekelezaji na jitihada za serikali na sekta binafsi katika kutokomeza magonjwa ya mifugo nchini na kuimarisha mazao yatokanayo na mifugo kiujumla.

Akizungumza Aprili 28, 2026 Jijini Arusha kwa Niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, wakati wa ufunguzi rasmi wa kikao cha kikanda cha kujadili namna ya kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya mifugo katika mipaka ya nchi, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agness Kisaka Meena amesema wizara imepokea dozi milioni mbili kutoka FAO ambazo zitasaidia katika kutokomeza ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo.

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ipo katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo, ambapo mwanzoni mwa kampeni ya chanjo kitaifa, FAO ilitoa kwa ukarimu dozi milioni 3.9 za chanjo, na leo imetoa dozi nyingine milioni 2." amesema Bi. Meena

Aidha, Bi. Meena amesema hapo awali serikali ilitenga shilingi bilioni 216 za kitanzania katika kipindi cha miaka mitano ijayo ili kusaidia shughuli za chanjo, utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo, na tayari, shilingi bilioni 69.2 zilitolewa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, na juhudi hizi zilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ili kuhakikisha magonjwa ya mifugo yanadhibitiwa na kutokomezwa kabisa.

Vilevile, Bi. Meena ameweka wazi Mpango Mkakati na Mfumo wa Kudhibiti Magonjwa ya Mifugo ambao unajadiliwa na wadau mbalimbali kwenye kikao hicho chenye lengo la kuangalia ni namna gani wanaweza kudhibiti na kutokomeza ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo ifikapo 2030, ikiwa na lengo la kuangalia chanzo chake na kudhibiti kwa kushirikiana na nchi jirani.

Pia, Bi. Meena amezishukuru taasisi mbalimbali zinazosaidi katika kupambana na magonjwa ya mifugo ikiwemo Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Shirika la Dunia la Afya ya Wanyama (WOAH) na Umoja wa Afrika - Ofisi ya

Rasilimali za Wanyama ya Afrika (AU-IBAR) kwa kutekeleza mipango inayokamilisha juhudi za serikali katika kudhibiti na hatimaye kutokomeza magonjwa hayo ya mifugo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Nchini, Dkt. Benezeth Lutege ameweka wazi ni kwa namna gani Tanzania imefanikiwa katika kupambana na kutokomeza magonjwa ya mifugo ikiwemo ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo baada ya Kampeni ya Chanjo ya Kitaifa ya awamu ya kwanza kufanyika, ambapo imefanikiwa kuwakinga mifugo kwa asilimia 80% katika kudhibiti magonjwa, kiasi kwamba ikifika mwaka 2030 mangojwa hayo yatakuwa yametokomezwa kabisa nchini.

Naye, Mwakilishi wa Shirika la Dunia la Afya ya Wanyama (WOAH) Kanda ya Afrika Mashariki, Dkt. Neo Maptise amesema wao kama shirika wamejizatiti katika kutokomeza magonjwa hayo ya Mifugo kwa kushirikiana na nchi mbalimbali katika kutafuta kiini cha chanzo cha magonjwa hayo na ndio maana wameandaa Mpango Mkakati wa kutokomeza magonjwa yanayowakumba mifugo.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agness Meena (aliyekaa katikati), akiwa pamoja na wadau mbalimbali wa sekta ya mifugo, baada ya kufungua Kikao cha kikanda cha kujadili namna ya kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya mifugo katika mipaka ya nchi, kilichofanyika Hoteli ya Maasai Land, Aprili 28, 2026 Jijini Arusha.



**MATANGAZO**

# BEI YA MBEGU ZA MALISHO
## (JUNCAO NA MAJANI TEMBO)

**Punguzo** — Hadi 90%

**SHILINGI ~~4,000~~ → Sh. 1000**

**Kwa mawasiliano zaidi:**

Vikuge (Pwani) - 0714060849
Langwira (Mbeya) - 0757637241
TALIRI - 0655420703
LITA - 0742762364

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Wizara ya Mifugo Na Uvuvi




**Kwa Mawasiliano Zaidi:**
Kingolwira (Morogoro) - **0787493792**
Mwamapuli (Tabora) - **0779154377**
Ruhila (Songea) - **0659669227**

www.mifugouvuvi.go.tz



# Jarida la Mtandaoni

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
vBarua Pepe : barua@mifugo.go.tz

@wizara ya Mifugo na Uvuvi